TANGAZO LA SERIKALI Na. 219 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MAPUTI YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Maputi ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M1 yenye majira - nukta 533499MS, 8826895KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $72^0$ 39'29'' kwa umbali wa kilomit1.8 hadi kwenye alama za mpaka ya upimaji namba M2 yenye majira - nukta 535185MS, 8827421KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $64^0$ 49'13'' kwa umbali wa kilomita 0.89 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M3 yenye majira - nukta 535989MS, 8827043KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $47^0$ 26'02'' kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M4 yenye majira - nukta 536963MS, 8826149KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa kufuata mto Mamba kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M5 yenye majira - nukta 534903MS, 8824045KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $26^0$ 13'41''kwa umbali wa kilomita 3.18 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*